**SOMO LA 13**

**SIKU YA HUKUMU**

"Ufalme ni kama mtu.. Baada ya muda mrefu, bwana yuaja, akafanya hesabu na watumishi hao.. Na kumweka mtumishi asiye na faida katika giza la nje."

Somo lililopita lilionyesha kuna jamii kubwa kutoka kwa vizazi vilivyopita, wengi wao wakiwa wanapumzika makaburini, ambao wanangojea uamuzi wa Mungu wa kukubaliwa au kukataliwa. Ni lini na jinsi gani uamuzi huu utatolewa?

Baadhi hujibu, 'Bwana awajua walio wake' (2 Timotheo 2:19), ikimaanisha humo kwamba hakuna umuhimu wa kusimama mbele ya kiti cha hukumu na kujibu; kwamba hatima ya wote tayari imeamuliwa katika akili ya Mungu. Ni kweli kwamba Mungu anajua, lakini hii haizuii kuweka muda na mahali palipo wazi, uchunguzi rasmi na tamko, kabla ya jeshi lote la walio "wajibika" ambao wamekusanywa kwa kusudi hili.

**NJIA ZA MUNGU ZAFUNUA HAKI YAKE**

Mungu hachukulii hivihivi ufahamu wake kwa kupuuza mpangilio wake wa mambo ambao unaonyesha watu haki na sababu zake. Shughuli zake zote na watu zimeundwa kudhihirisha na kutangaza na kufundisha. Anajua mwisho kutoka mwanzo, na anaweza kuruka hadi mwisho ikiwa atachagua, lakini hii haitakamilisha kusudi lake pindi watu wanapohusika.

Kwa nini, kwa mfano, aliruhusu kizazi kisicho cha uaminifu cha Waisraeli kuhepa Misri chini ya uongozi wa Musa, na akawa na subira ya muda mrefu kwa uovu na uasi wao, kabla ya kuwaangamiza jangwani? Kwa nini hakuwaangamiza tu mara moja? Alijua tokea mwanzo kuwa watakuwa waovu na wasio na maana. Tunaona mengi yalitimizwa kwa utaratibu alioufuata, kwa watu waliokuwepo wakati ule na kizazi cha baadaye. Kiti cha hukumu kitafuata mkondo huu.

Na kwa nini kwa muda mrefu aliwavumilia Wayahudi katika ukaidi wao wa mara kwa mara – akijua kuwa watawakataa wajumbe wake wote, na mwishowe Mwana wake mwenyewe? Na kwa nini watu kama vile Anania na Safira waliletwa mbele ya mitume, na hatia yao kuletwa na ushahidi wao, kabla ya kuangamizwa? (Matendo 5: 1-11). Hakika uhalali wa mchakato huo ni dhahiri : na hukumu hali kadhalika.

Pia hapa kuna kazi muhimu sana ya kanuni ya Mungu ya mapenzi ya bure na uchaguzi huria. Ingawa Mungu, kwa Ujuzi wake anajua mwisho kutoka kwa mwanzo, haweki kizuizi cho chote ila anamwacha kila mtu afanye maenzi yake kwa kuchagua la kufanya kwa mujibu wa dhamira yake. Kila mtu anawajibikia matendo yake, mema au mabaya na ni muhimu kwa mpango wa Mungu kwamba kanuni hii haitiliwi vikwazo katika utekelezaji wake. Tunapokuwa na ujuzi wa kusudi la Mungu, na kujua kinachompendeza na yale yasiyompendeza, tunakuwa na WAJIBU; na kila mtu anayewajibika atahukumiwa kwa msingi wa jinsi walivyotekeleza mapenzi yao katika chagizo la maisha haya ya sasa.

WAAMINIFU WATASHANGILIA KUWA NDIVYO ILIVYO

Ni kweli Mungu anajua, lakini je, si vema kuwaonyesha waziwazi wanaowajibika msingi ambao umetumiwa ili kuwakubali au kuwakataa? Mbali na kutoa sababu ya kulitetea jambo hili, ni hatari kwa vyo vyote vile, kukataa kanuni iliyotangazwa ya kimsingi na ya kweli: siku ya mwisho ya hukumu Kristo atakaporudi - kama ilivyoonyeshwa katika masomo yaliyopita.

Kwa wale ambao, katika maisha haya, wamefanya kazi kwa uaminifu na uvumilivu katika kukabiliana na udhalimu na upotofu,ni jambo la farija kujua kutakuwa hatimaye na tume isiyo na dosari ya wazi, kadamnazi ya watu, kurekebisha kila kosa.

Na ni faraja kujua kwamba kati ya huu udhalimu, ushindi wa dhambi, nyakati za maovu, na utukufu, ukamilifu wa haki wa Ufalme, kutakuwepo uchunguzi ambao, kwa uthibitisho wa Mungu, utazuia kuingia kwa kitu chochote kilichonajisi, chochote kinachojidai kuwa na fahari ya binadamu. Mateso haramu yatalipizwa kisasi mbele ya watu, uaminifu ambao haujawai kuonekana utakubaliwa, Karama isiyothaminiwa itadhihirishwa hatimaye, kila ovu la siri litafichuliwa kuwekwa wazi na kuadhibiwa na kuondolewa katika hali inayostahili..

Lengo la hukumu ni kumpa kila anayostaili, mema au mabaya, haki yao –

"Wengi watasema katika Siku ile, Bwana, Bwana, nk… nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu , ninyi mtendao maovu "(Mathayo 7:22 23).

"Kila neno lisilo maana, watakalolinena wanadamu, watatoa hesabu ya neno hilo siku ya hukumu" (Mathayo. 12:36).

"Kila mtu miongoni mwetu atatoa habari zake mwenyewe mbele ya Mungu" (Warumi 14:12).

MIFANO MINGI INAONYESHA KITI CHA HUKUMU

Ushahidi mwingine muhimu ni unapatikana kwa mifano ya Kristo. Katika mifano hii, anaonyesha uhusiano kati yake mwenyewe na watumishi wake, kuhusiana na kuondoka kwake kwa kipindi fulani> kutoka duniani, na baadaye kurudi. Mifano michache itatosha kutoa pointi:

1) **Mfano wa kabaila ambaye alikwenda nchi ya mbali kupokea mamlaka ya Ufalme –** "Wakati aliporudi ameupata ufalme wake, aliamuru waitwe wale watumwa wake… ili ajue faida aliyopata kila mtu kwa biashara yake."(Luka 19:15).
   Angalia kwa makini kuwa sio tu suala la 'viwango vya malipo' (kama wengi wanavyotolea ubishi, huku wakijitahidi kuhepuka na suala la ukweli wa Mungu wa uchunguzi huo wa kina). Cha msingi ni suala la kukubalika au kukataliwa: watumishi wawili walipongezwa na kupewa tuzo; wa tatu alinyang’anywa kile alichokuwa nacho (Luka 19:26).

2) Mfano wa 'mkusanyiko wa watumishi kutoa hesabu': wawili tena wanapewa zawadi, na wa tatu – ‘mtumishi asiye na faida' - 'anatupwa katika giza la nje "(Mathayo 25:30): hakuna uwezekano hapa wa kupotosha wa 'viwango tofauti vya malipo.’
3) Mfano wa mfalme kuwakaribisha wageni kwenye harusi ya mwanawe ( 'karamu ya mwana kondoo' - Ufunuo 19: 9): Wakati wageni walikuwa wamekusanyika, mfalme anawakagua ili kuhakikisha kuwa Wamevaa kwa njia inayokubalika. Mmoja anapatikana bila vazi la arusi, na 'anafungwa mikono na miguu, na kutupwa katika giza la nje "(Mathayo 22:14). Tena, hakuna 'kiasi cha malipo' lakini kukataliwa.
4) Mfano wa wavu uliotupwa baharini: Wakati ulipojaa (mwito kamili ulipokamilika), waliuvuta pwani na kukagua samaki wema na wabaya – ‘akitupa wabaya MBALI' (Mathayo 13:48) - siyo tu kuwapa zawadi ndogo.
**5)** Mfano wa watumishi wanaosubiri kurudi kwa Bwana wao, Bwana alikuja ghafla (kama Kristo mara nyingi anavyoonya), na kugundua mmoja wao si mwaminifu, na 'atamkata vipande viwili "(Luka 12:46) - vigumu kutafsirika kama kumuzawadi tu yeye kidogo.
6) Mfano Wa Wasichana Kumi wanaomsubiri bwana arusi, bwana arusi akaja; wenye busara wakaingia ndani pamoja naye arusini; wajinga wanatengwa na mlango unafungwa, Bwana harusi akawajibu mlango ukiwa umefungwa, ‘Siwajui ninyi (Mathayo 25:12).

'Wengi wanaitwa’ asema Yesu, 'lakini wachache wanateuliwa.” (Mathayo 20:16). Lini na kwa njia ipi "walioteuliwa" walitengwa na "walioitwa"? Mifano hii yote yatoa jibu –

"Atakayewahukumu walio hai na waliokufa, kwa kufunuliwa kwake na Ufalme wake" (2 Timotheo 4: 1)

WEMA NA WAOVU WATAAMKA NA KUHUKUMIWA PAMOJA

Baadhi wanasema ni waovu tu wanaoishi ambao wataalikwa mbele ya kiti cha hukumu na kuadhabiwa:: kizazi cha walio hai wakati wa kurudi kwake Kristo.

Lakini Danieli na Kristo wanakubaliana wanaposhuhudia kwamba wakati Kristo atakapokuja wafu watafufuliwa, baadhi wapate utukufu, na wengine aibu; baadhi wapate uzima wa milele, wengine hukumu (Daniel 12: 2: Yohana 5:29).

Paulo anasema:

"Msihukumu neno kabla ya wakati wake, hata ajapo Bwana; ambaye atayamulikisha yaliyositirika ya giza .., Ndipo kila mtu atakapoipata sifa yake kwa Mungu..." (1 Wakorintho 4: 5).

'Mambo ya giza' na 'sifa ya Mungu' yote yatafunuliwa kwa wakati mmoja - wakati 'Bwana atakaporudi.' Paulo anasema zaidi (2 Wakorintho 5:10) kuwa katika kiti cha hukumu cha Kristo (ambapo ‘sote’ lazima tusimame) tutapokea katika mwili ‘mema au **MABAYA’**. Katika barua yake kwa Warumi anasema (2: 6,9,16) kwamba ‘matendo mema’ yatalipwa na 'uzima wa milele' na kutotii kutalipwa na 'Mateso na maumivu' kwa wakati mmoja –

" katika siku Mungu atakapohukumu mambo ya siri ya wanadamu kulingana na Injili yangu.”

Ni dhahiri kuwa kiti cha hukumu cha Kristo ni mstari mkubwa ya kuweka mpaka kati ya muda wa majaribio na utukufu; wakati uliowekwa kuonyesha nani ni nani, na kutenganisha wenye haki na wasio haki. Maneno ya Kristo, kote katika mwanzo wa huduma yake (Mathayo 7:22) na mwisho (Mathayo 25: 37-44) yanaonyesha suala haijulikani mpaka badaye: wenye haki hawana uhakika wa kukubaliwa kwao hadi hapo, na waovu wanashangazwa kukataliwa kwao.

Wote, kwa hivyo, ni lazima wasimame mbele ya kiti cha hukumu kwa pamoja katika hali ya kimwili na wanahusika kwa kupokea uzima wa milele au mauti ya milele. Hawawezi kuwa na mwili wa uzima wa milele mpaka baada ya kuonekana mbele ya kiti cha hukumu.

Wazo, basi, kuwa wenye haki waliokufa huruka kutoka kaburini mara moja na kuingia katika maisha ya uzima wa milele (una msingi tu juu ya tafsiri potofu za 1 Wakorintho 15:52, "alimfufua katika hali ya kutoharibika ') haiambatani na picha ambayo imerudiwa mara nyingi, na mara kwa mara ya maandiko matakatifu yote. Yote mazuri na mabaya yanapokelewa 'katika mwili' (2 Wakorintho 5:10, kwa kuondoa mambo yasiyo sahihi) katika kiti cha hukumu.

BAADHI YA VIFUNGU VIGUMU?

Sio vifungu vyote vitakuwa wazi au vya kueleweka moja kwa moja kama zile tumezingatia. Tunapokutana na kifungu ambacho hakionekani kusema kitu sawia nasi, kabla ya kurukia hitimisho ni lazima kuwa makini kuzingatia mazingira na Mada ya kifungu. Unakumbuka kanuni za ufafanuzi wa Biblia ambazo tulisoma katika masomo yaliyopita. Hebu tuangalie mifano michache:

Mfano # 1: Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza (1 Wathesalonike 4 : 16)

"Waliokufa katika Kristo watafufuliwa KWANZA" inaonekana kuunga mkono dhana ya kwamba wenye haki waliokufa wanafufuka kabla ya wafu wasio haki, wa mwisho wakifufuliwa baadaye. Tumeona, hata hivyo, kwamba wanafufuliwa na kusimama mbele ya kiti cha hukumu kwa pamoja. ‘Kufufuliwa hapa kwanza' iliyotajwa inahusiana na kuchukuliwa kwa walio na maisha, kama mazingira yanavyoonyesha wazi. Paulo anashughulikia uhusiano kati wafu wenye haki na walio hai wenye haki. Hawazi kuwahusu waovu kabisa, ambao sio wenye maana katika mpango wa milele wa Mungu. Anawahakikishia wasomaji waombolezaji wake kwamba wafu hawana hasara; wanafufuliwa kabla ya walio na maisha kuchukuliwa. Waovu wanapuuzwa katika vifungu vingi, kama kote katika 1 Wakorintho 15. Hii ina busara, lakini wametajwa vya kutosha kutoa picha halisi, na kuamka kwao kwa pamoja na kuhukumiwa pamoja na wenye haki itabainika mahali pengine.

Mfano # 2: Heri na mtakatifu ni yeye aliye na sehemu katika ufufuo wa kwanza; juu ya hao mauti ya pili haina nguvu, bali watakuwa makuhani wa Mungu na wa Kristo, nao watatawala pamoja naye kwa miaka elfu moja. (Ufunuo 20: 6)
Hii inaweza kuonekana kama inasema kwamba kama wale ambao wana sehemu katika ufufuo wa kwanza ni "heri na watakatifu", kisha "waovu" hawafufuliwi. Lakini hakuna kitu hapa kupinga ufufuo na hukumu ya wasio na haki. 'Kuwa na sehemu' inamaanisha kupokea zawadi na sehemu katika ufufuo huo, yaani, kuwa tusigeuzwe mbali na Kristo. Biblia inafundisha kuwa kuna ufufuo mara mbili. Ya kwanza 'ni ufufuo unaotokea Kristo atakaporudi. Ufufuo wa pili unafanyika mwishoni mwa miaka ya 1000. Tazama mstari wa 5 - 'wengine waliokufa' ambao 'hawaishi tena mpaka miaka 1000 ziishe' inahusu wote wanaokufa baada ya kurejea kwa Kristo wakati wa miaka 1000 wa muda wa Ufalme: yaani, hakuna ufufuo zaidi hadi mwisho wa Milenia.

**LAZIMA TUSAWAZISHE SHUHUDA ZOTE**

Mfano # 3: ... mbiu itakapolia, na wafu watafufuliwa, wasiwe na uharibifu, nasi tutabadilika. (1 Wakorintho 15:52)
Paulo anaposema kuwa 'wafu watafufuliwa katika hali ya kutokufa, hayapingi mafunzo yake mwenyewe yaliyoongozwa kwa pumzi ya Mungu kimaandiko, na maneno ya Kristo, kuwa wafu watafufuliwa, na kukusanywa mbele ya hukumu, kuhukumiwa na kisha (kama anastahili) kuzawadiwa kwa uzima wa milele. Ni muhimu kutambua kuwa hataji hukumu katika sura hii wakati wote.

Je anatuwasilisha na dhana tofauti hapa kuliko mahali pengine? Bila shaka hapana. Ni lazima kuzileta zote pamoja, na kutenga nafasi kwa masuala yote, ingawa baadhi hazijatajwa hapa. Kujaza maelezo, ni lazima kuweka hukumu katika nafasi ambapo yeye mahali pengine anasema inatakikana. Kumbuka v.45 ( "muktadha") –
"Mtu wa kwanza, Adamu, akawa nafsi iliyo hai: Adamu wa mwisho (Kristo) ni roho yenye kuhuisha."
Kama hatungekuwa na taarifa kutoka sehemu nyingine ya maandiko, na kutupatia na historia nzima ya mchakato wa kuzaliwa kwa Kristo na ukuaji na maisha na kifo, kufuatia ambayo utukufu katika 'kufurukuta roho' ilifanyika, tutadhania kwa kawaida > kutokana na kifungu hiki kwamba alianza kama 'roho ya kufurukuta,' kama vile Adamu alivyoanza kama 'nafsi hai.'
Hata hivyo, wakati tunapochunguza picha kamili kama ilivyotolewa kwa njia ya kuleta pamoja kwa sura mbalimbali hatutaanguka katika kosa hilo, kwa sababu tuko makini na maelezo hayo tuliyopewa mahali pengine.
Wala hatutajiingiza katika makosa ya kufikiri 'kufufuliwa katika hali ya kutoharibiwa' ni tukio la papo kwa hapo, mara moja pindi wanapotoka kwenye makaburi, kukwepa kiti

cha hukumu cha Mungu. Kwa ufupi, maelezo kwa ujumla hayapuuzi au kutenga maelezo yanayoshirikishwa mahali pengine katika maandiko.

HAPANA " MTU ANAYEWAJIBIKA" ATAKAYEEPUKA HUKUMU Hebu tukumbuke milele: Kuna 'Siku' iliyoteuliwa wakati 'Mungu atahukumu siri za binadamu kupitia kwa Yesu Kristo "(Warumi 2:16). Hakuna mwenye ujuzi wa kusudi la Mungu anayeweza kuepuka hayo. Wote watakuwa huko ambao Mungu anazingatia wana ufahamu wa kutosha wa mapenzi yake kuwajibika na kujibu na ndiyo uamuzi Mungu pekee anaweza kufanya hivyo kwa mtu binafsi. Hakuna kile kitakachokuwa **siri**. ‘Siri zote za binadamu' zitaanikwa wazi kwa ajili ya kutafuta kuangaazwa na nuru - ila, bila shaka, mambo yatakayokuwa kweli wametubu kwayo, na kutia jitihadi dhidi yake, na kusamehewa, na katika rehema 'kufutiliambali'.

Hii ni faraja ya daima kwa wale ambao daima wanajitahidi kuwa waaminifu na wenye haki na kumpendeza Mungu. Lazima iwe onyo daima kwa wale ambao hawajaweka, na kudumishwa, katika njia ya uaminifu na haki. Ibada ya jumla na huduma katika siku hii fupi sana ya muda wa majaribio itamaanisha kukwepa kaburi lililo baridi, ili kuepuka siku ya mwisho ya kutisha ya adhabu kwa wanaokaidi, na utukufu na furaha pamoja na Mungu milele na milele. Nani ataweza kuwa mjinga ili asifanye uamuzi wa busara? Ukingoja kesho, utapitwa na mambo..

**MASWALI KWA SOMO LA 13**

1. Nini kanuni gani ya Mungu inayoonyesha umuhimu wa hukumu ya Kristo kufanyika katika hali iliyo wazi ili kuwazawadi waliokusanywa?

2. Kwa nini Mungu hakuharibu kizazi cha waovu kule Misri bila maelezo?

3. Mfano gani katika Agano Jipya inaeleza kanuni ya kuitwa kutoa hesabu?

4. Misemo gani ya Kristo zinaonyesha kuwa uamuzi haujulikani kwa wapokeaji hadi baada ya mahojiano na hukumu?

5. Ni Lini ambapo tutatoa hesabu ya kila neno tunalotamka?

6. Ni katika maandiko gani ndipo Danieli anasema wafu watafufuliwa pamoja, wengine wapate uzima wa milele wengine aibu?

7. Katika kifungu gani ndipo Kristo anasema wafu watafufuliwa kwa pamoja, baadhi kwa maisha na wengine kuhukumiwa?

8. Katika mandiko yapi ndipo Paulo anasema ni lazima sote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo?

9. Sura gani mbili katika Luka, na sura mbili katika Mathayo zinatoa mifano inayowakilisha kurudi kwa Kristo, kwa kuwahukumu wanaowajibika na kukataa waovu (kabaila, watumishi wanaosubiri, arusi ya mwana, wanawali 10, talanta)?

10. Katika kifungu kipi ndipo Paulo anasema, 'msihukumu kabla ya WAKATI' (wakati Kristo atakuja kuleta mwanga yote ya 'giza' na 'sifa')?

11. ‘Wafu katika Kristo watafufuliwa MWANZO’ kuhusiana na gani nyingine?

12. a) Inamaanisha nini kuwa 'na sehemu' katika ufufuo wa kwanza?

b) Je, mtu anaweza kufufuliwa katika 'ufufuo wa kwanza' pasipo kupata 'sehemu' au zawadi ndani yake?

13. ‘Wengine kati ya waliokufa’ wasioishi hadi mwisho wa miaka 1000 ni akina nani?

14. Ni kanuni gani nzuri ya tafsiri ambayo huzuia mmoja katika kufanya makosa ya kudhania kuwa waliokufa wanafufuliwa wakiwa katika kutoharibika ?

15. a) Ni lini ambapo Kristo alifanywa ‘roho ya kuhuisha'?

b) Je, tunajifunza hili kutoka kwa 1 Wakorintho. 15 pekee?